# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 010 OKTOBA 2021

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



## 1 MHE. WAITARA AMEITAKA TMA KUBORESHA MAZINGIRA CHUO CHA HALI YA HEWA

## 2 DKT. KIJAZI AONGOZA UJUMBE WA TANZANIA KATIKA MKUTANO MKUU MAALUMU WA KIDUNIA WA HALI YA HEWA



## 3 FAHAMU ZAIDI: MISIMU YA MVUA NCHINI



KITAIFA

# MHE. WAITARA AMEITAKA TMA KUBORESHA MAZINGIRA CHUO CHA HALI YA HEWA

**Dar es Salaam**



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi(Sekta ya Uchukuzi), Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara (MB) ameitaka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuwekeza zaidi katika kuboresha mazingira ya chuo cha hali ya hewa kilichopo Kigoma.

Hayo yalizungumzwa katika ziara ya Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi iliyofanyika katika ofisi za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Ubungo Plaza, Tarehe 04/10/2021. Lengo la ziara hiyo ni kuifahamu TMA, kazi wanazofanya na kutambua changamoto za kiutendaji ili kuweza kufanya maboresho stahiki.

"Nilipokwenda Chuo cha hali ya hewa Kigoma niliona mazingira yake sio mazuri pamoja na kuwa Chuo hicho kipo katika ukarabati kinahitaji kiwe na mazingira mazuri kutokana na kuwa ndio chou pekee kinachotoa mafunzo ya awali ya hali ya hewa hapa nchini. Nafikiri mwenyekiti wa bodi na Mkurugenzi Mkuu mnapaswa kuwekeza pale" Alizungumza Mhe. Waitara.

Mheshimiwa Naibu Waziri aliongezea kuwa Mamlaka inajukumu kubwa kwasababu taarifa za hali ya hewa zinatumika katika sekta zote za maendeleo hapa nchini. Mwekezaji akitaka kuwekeza lazima afuatilie taarifa za hali ya hewa ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha aliwapongeza TMA kwa kazi nzuri wanazozifanya na kuwataka waendelee kufanya kazi kwa weledi wakijua kwamba kazi wanazozifanya zina mchango mkubwa katika

maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini. "Nawapongeza kwa kuboresha huduma za hali ya hewa hapa nchini na pia kuifanya Tanzania iendelee kung'ara katika Nyanja za kimataifa kwenye sekta ya hali ya hewa. Aliongeza Mhe. Waitara.

Mhe. Waitara aliahidi kwamba katika utaratibu wa kuboresha maslahi ya watumishi kama alivyoahidi Mhe. Rais watumishi wa TMA wataboreshewa Maslahi yao ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi.

Awali, wakati akimkaribisha Mhe. Naibu Waziri, Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Dkt. Buruhani Nyenzi kupitia taarifa yake fupi alisema kuwa Mamlaka imeanza kuifanyia kazi changamoto ya vifaa ambapo Serikali imeendelea kutenga fedha kwaajili ya ununuzi wa vifaa vya hali ya hewa. Changamoto ya maslahi duni nayo pia imeanza kufanyiwa kazi ambapo 'Job Evaluation' imefanyika kwa kutumia Chuo cha Utumishi wa Umma na mapendekezo ya mishahara stahiki kwa wafanyakazi yamewasilishwa katika Mamlaka husika.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani, Dkt. Agnes Kijazi alishukuru Serikali, "Napenda kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwani imeendelea kuiwezesha Mamlaka kuwa na vitendea kazi vya kisasa na wataalamu bingwa ambao wanapatiwa mafunzo mara kwa mara kwa lengo la kuwaongeza ujuzi". Alisema Dkt. Kijazi. Aliongeza kusema "Nichukue fursa hii adhimu kuishukuru Serikali yetu kupitia Wizara kwa kutupatia Rada nyingine mbili ambazo ukamilikaji wake utapelekea kufikiwa kwa malengo ya muda mrefu ya kuwa na Rada 7 za hali ya hewa kwa nchi nzima".

Alimalizia kwa kumhakikisha Mhe. Naibu Waziri kwamba maelekezo yote aliyoyatoa hususani uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma yatawekewa mpango mkakati wa utekelezaji.



KIMATAIFA

# DKT. KIJAZI AONGOZA UJUMBE WA TANZANIA KATIKA MKUTANO MKUU MAALUMU WA KIDUNIA

**Dar es Salaam**



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi ameongoza ujumbe wa Tanzania katika mkutano mkuu maalumu wa Kidunia wa hali ya hewa "Extra-ordinary session of the World Meteorological Congress (Cg-Ext (2021), uliofanyika kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 11 hadi 22 Oktoba, 2021.

Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadili utekelezaji wa maamuzi ya mkutano mkuu wa 18 wa Kidunia wa hali ya hewa "Eighteenth Session of the

World Meteorological Congress (Cg-18)" uliofanyika mwaka 2019, pamoja na mapendekezo mapya ya kuboresha zaidi huduma za hali ya hewa ili ziweze kuleta tija zaidi kwa jamii. Mkutano mkuu huo maalumu ulijielekeza zaidi katika maeneo makuu matatu, ambayo ni:

- Tathmini ya utekelezaji wa mabadiliko ya muundo wa WMO "(WMO reform)";
- Mchango wa WMO katika maendeleo ya sekta ya maji (WMO support to the global water agenda); na
- Maboresho ya sera ya WMO ya ubadilishanaji wa data za hali ya hewa (WMO Unified Policy on International Data Exchange).

Mkutano huo ulipokea na kujadili taarifa na mapendekezo ya kamati na vikosikazi mbalimbali vya WMO vinavyoshughulikia maeneo hayo.

Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni mapendekezo ya Kikosi kazi cha WMO kilichopewa jukumu la kufanya mapitio ya muundo na utendaji kazi wa kanda za WMO (Executive Council Task Force on the Comprehensive Review of the WMO Regional Concept and Approaches). Dkt. Kijazi ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kikosikazi, aliwasilisha maapendekezo ya Kikosikazi hicho kuhusiana na maboresho ya kimuundo na utendaji kazi wa kanda za WMO, ili ziweze kushiriki ipasavyo katika uboreshaji wa huduma za hali ya hewa kwa Nchi Wanachama wa WMO zilizomo katika kanda husika. Mkutano ulipitisha mapendekezo yaliyowasilishwa na kumwomba Katibu Mkuu wa WMO kusimamia utekelezaji wa maamuzi hayo.

Ujumbe wa Tanzania katika mkutano mkuu huo maalumu wa Kidunia wa hali ya hewa ulijumuisha washiriki kutoka TMA, Wizara ya Maji, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Ofisi ya Umoja wa Mataifa, Geneva – Uswisi.

Mkutano mkuu huo maalumu ulifuatiwa na Mkutano wa 74 wa Baraza Kuu la Utendaji la WMO "Seventy- Second Session of the WMO Executive Council (EC-74) uliofanyika pia kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 25 hadi 29 Oktoba, 2021 kwa lengo la kujadili utekelezaji wa maamuzi ya mkutano mkuu maalumu wa Kidunia wa hali ya hewa. Mikutano yote miwili iliongozwa na Rais wa WMO, Prof. Gerhard Adrian, ambaye ni raia wa Ujerumani.

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## MISIMU YA MVUA NCHINI

Mvua za msimu nchini na eneo zima la Ukanda wa Afrika Mashariki zinatokana na mjongeo wa Kaskazini-Kusini wa ukanda wa mvua (Intetropical Convergence Zone, ITCZ). Kawaida, ukanda wa mvua huhamia kusini kupitia Tanzania miezi ya Oktoba hadi Disemba (OND), na kufikia kusini mwa nchi miezi ya Januari na Februari na kurudi Kaskazini kipindi cha Machi hadi Mei (MAM). Hali hii husababisha baadhi ya maeneo kupata vipindi viwili tofauti vya mvua.

Aidha, kujongea huku kwa ukanda wa mvua husababisha pia baadhi ya maeneo kupata msimu mmoja wa mvua unaoanza mwezi Novemba na kuisha mwezi Aprili au Mei ya mwaka unaofuata.

**PICHA** | **MAELEZO**



### MSIMU WA MVUA ZA MASIKA

- Huu ni Msimu wa Mvua unaotokea miezi ya Machi hadi Mei katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam na Tanga, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko).



### MSIMU WA MVUA ZA VULI

- Huu ni Msimu wa Mvua unaotokea miezi ya Oktoba hadi Disemba katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam na Tanga, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko).



### MVUA ZA MSIMU

- Huu ni Msimu wa Mvua unaotokea mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa maeneo ya ukanda wa magharibi (mikoa ya Kigoma, Tabora, Rukwa na Katavi), ukanda wa kati (mikoa ya Singida na Dodoma), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe), kusini mwa nchi (mkoa wa Ruvuma), ukanda wa pwani ya kusini (Mikoa ya Lindi na Mtwara) pamoja na maeneo yaliyoko kusini mwa mkoa wa Morogoro.

# KISWAHILI CHETU

## ISTILAHI ZA HALI YA HEWA

Tuangazie herufi L & M:

| | |
|---|---|
| local or community transmission | maambukizi ya ndani |
| lockdown | zuio la kutotoka nyumbani |
| locked in | zuiwa ndani |
| mask | barakoa |
| medical ventilator | kipumulishi cha kitabibu |



kipumulishi cha kitabibu


JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 008
AGOSTI, 2021
1 BODI YAWATAKA WADAU WA HALI YA HEWA KUTOA USHIRIKIANO MZURI KWA TMA
2 DKT. KIJAZI AELEZA FAIDA KWA NCHI WANACHAMA WA WMO KANDA YA AFRIKA
3 FAHAMU ZAIDI: MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTABIRI WA HALI MBAYA YA HEWA WA SIKU TANO

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**


**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Kennedy Mgeta
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa
Kituo Kikuu cha Utabiri


www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline TV


Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
388 Br. Morogoro
S.L.P 3056,
16102 Dar es Salaam, Tanzania.